



Maswali Na majibu (Myths)

Q. Ukimwi ina dawa?

Hapana. Kuna matibabu ambayo husaidia mtu kuishi maisha marefu lakini hakuna dawa ya ukimwi.

Q. Kufanya mapenzi na mtu ambaye bado hajafanya mapenzi huonya mtu?

La . hii haisaidi kwani utamwambukizia virusi hivi vya ukimwi.

Q. Naweza pata virusi vya ukimwi kwa kukaa karibu na watu wenye ugonjwa wa ukimwi.

Kuna njia tatu za kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi: kwa kufanya mapenzi na mtu mwenye ugonjwa huu , kwa kwa damu na kutoka kwa mama hadi mwanaye ambaye hajazaliwa. Kuwa karibu na watu wenye virusi vya ukimwi haina hatari yoyote – kula chakula pamoja, kuvaa nguo pamoja , kushikana mikono haina hatari yoyote.

Q. Watu wnye virusi vya ukimwi wanaweza pata watoto?

Ndio. Wamama wenye virusi wanaweza pata matibabu ambayo inaweza saidia wanao wasipate virusi vya ukimwi , kujua hali yako ni muhimu sana wakati mama ana mimba.

Q. Nikipatikana na virusi nini itafanyika?

Kwanza kupatikana na virusi haimaanishi utakufa kwa haraka , watu wengi wenye virusi huisha maisha marefu na yenye afya. Ni vizuri kujua hali yetu ili tuweze kuchunga wale tunaishi nao. Matibabu husaidia mtu kuishi maisha marefu.

Q. Watu wawili ambao wana virusi vya ukimwi wakifanya mapenzi hii inajalisha?

Ndio .Aina tofauti ya virusi inaweza pitishwa kwa mtu mmoja hadi mwingine na hii inaongeza nambari ya virusi mwilini na ni ngumu sana kutibu.

Q. Nimeolewa , kwa hivyo siwzi pata virusi .

Hii si ukweli , mmoja wenu anaweza kuwa alikuwa na virusi kabla hamjaoana ama anaweza pata virusi hivi mkiwa bado mumeoana kwa kupitia njia mingi .kupimwa ni muhimu sana ili kujua hali yako na mwenzako.

Q. Virusi vinaenezwa na mbu?

A.La.

Q. Wanaume wanaweza ambukizwa virusi na wanawake?

Ndio. wanaume wanaweza ambukizwa virusi na wanawake wakati wa kufanya mapenzi.